# DUA

kutunga
Dr. Abdul-Muhsin Ibnu Muhammad Al-Qaasim
Imamu Na Hatibu Wa Msikiti Mtukufu Wa Mtum

# DUA

**KWA KUTEREMSHA KITABU HICHI PANGUSA KODI**

a-alqasim.com

# DUA

**Dr. Abdul-Muhsin Ibnu Muhammad Al-Qaasim**

Imamu Na Hatibu Wa Msikiti Mtukufu Wa Mtum

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah Mola Mlezi wa walimwengu, na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, watu wake, na masahaba wake wote, ama baada ya himdi hii:

Basi Allah ameumba viumbe wazito wawili [binadamu na majini] kwa ajili ya kumuabudu Yeye, na ni katika fadhila za Allah juu ya waja wake kuwa ameweka ibada tofauti tofauti, basi miongoni mwake ni ibada ambazo ni za kimoyo, kama vile Tawakkul [kumtegemea Allah], na kumuhofu Allah, na miongoni mwazo ni ibada za Dhahiri, kama vile Swala na Zaka, na kiini cha ibada na mtakaso wake ni Dua [Maombi], basi shani yake katika Dini ni kubwa, na zimekuja kwa winigi dalili za kubainisha cheo chake, za kuwahimiza watu nayo na za kubainisha adabu zake.

Nayo ni ibada ambayo waja hawakosi kuihitajia, Pamoja na tofauti katika hali zao na vyeo vyao, na atakayekuwa na ikhlasi katika Dua yake, na akawa ameafiki ndani yake sunnah ya Nabii wake swala na salamu za Allah zimshukie; atakuwa ametekeleza

ibada tukufu, na Dua yake itakuwa ni yenye matarajio zaidi ya kukubaliwa, na ambaye atateleza akawa na kasoro katika kumuomba Allah aliyetukuka, au akavuka mipaka ndani yake, au moyo wake ukafungamana na asiyekuwa Yeye [Allah]; basi hakika huyo amehasirika katika ibada tukufu, na matakwa yake hayatotimia, na ataingia katika makemeo ya Allah.

Na kwa ajili ya umuhimu wa ibada na kuihitajia kwa watu; ndio nimeandika katika kitabu hichi vifungu ambavyo vinazunguka juu ya kutoombwa ila Allah peke yake, na nikakiita ((**Dua**)), na asili yake ni hutuba ya ijumaa nilioitoa katika Msikiti wa Mtume siku ya ijumaa, tarehe ishirini ya mwezi wa Swafar, mwaka elfu moja mia nne na arobaini na nne hijria.

Namuomba Allah akijaalie ni kilichofanywa kwa ikhlasi kukusudia Uso wake, na chenye kunufaisha waja wake.

**Na swala na salamu za Allah zimshukie Nabii Muhammad, jamaa zake na Masahaba wake wote.**

***Dr. Abdul-Muhsin Ibnu Muhammad Al-Qaasim***

***Imamu Na Hatibu Wa Msikiti Mtukufu Wa Mtume.***

***Nilikimaliza tarehe ishirini ya mwezi wa Safar, mwaka elfu moja mia nne na arobaini na nne hijria.***

# UHAKIKA WA DINI YA UISILAMU NI KUMTAKASIA ALLAH AMALI

Dini ya Allah aliyoiridhia kwa waja wote wa mwanzo wao na wa mwisho wao ni Uisilamu, Manabii wote walikuja nayo, na Mitume wote walibeba bendera yake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلۡإِسۡلَٰمُ﴾

{Bila ya shaka Dini mbele ya Allah ni Uislamu} [Aalu Imraan: 19]

Nao [Uisilamu] ni kuutakasa uso wako kwa Allah peke yake, na kusalimu kwake kuwa Yeye ni Mola, Mmiliki, Muendeshaji [wa kila jambo], na Ilahi Muabudiwa peke yake pasina wengine.

Nao [Uisilamu] ndio Al-Haniifiyyah ambayo ni mila ya baba yetu Ibrahim [salamu zimshukie], [Allah aliyetukuka amesema:]

﴿ثُمَّ أَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡكَ أَنِ ٱتَّبِعۡ مِلَّةَ إِبۡرَٰهِيمَ حَنِيفٗاۖ وَمَا كَانَ مِنَ ٱلۡمُشۡرِكِينَ﴾

{Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim aliyestakimu katika amri ya Allah, wala hakuwa miongoni mwa washirikina} [An-Nahl: 123].

Nao [Uisilamu] ni itikadi na sheria, na elimu na amali, na dhahiri inayosadikisha batini.

Na «laa ilaaha illa llaah» ndio msingi wake na asili yake, na mwanzo wake na mwisho wake, na sababu yake na lengo lake, na ndio kuba la jengo lake ambalo kwalo ndio unapatikana ukamilifu wake na uzuri wake.

Na cheo cha maana yake katika matamshi yake ni kama cheo cha roho katika mwili, hakupatikani manufaa ya mwili bila roho.

Na kuitamka bila ya kuitakidi maana yake hakumnufaishi mtu kitu.

Nayo [laa ilaaha illa llahu] ni neno lililokusanya Dini yote, atakayelisema hali akiwa mjuzi wa maana yake, mwenye kutenda kwa mujibu wake, na mwenye kutekeleza haki zake, basi atakuwa ametekeleza Tawhidi kiukamilifu, na atakaye tekeleza Tawhidi ipasavyo kama alivyoifaradhisha Allah ataingia Peponi bila hesabu wala adhabu.

# DINI YA UISILAMU IMESIMAMA JUU YA KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE

Dalili ya kweli kabisa kutoka kwa mja juu ya Tawhidi, na lenye kujulisha zaidi umahususi wa Muumba wa kupwekeshwa, ni kumuomba Allah peke yake pasina wengine, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema:

(**إِذَا سَأَلْتَ فَاسْأَلِ اللَّهَ**) رواه الترمذي.

(**unapoomba basi muombe Allah**) imepokewa na At-Tirmidhii[1].

Na Dini ya Allah haisimami isipokuwa juu ya kumpwekesha Allah kwa maombi pasina wengine, na kwa ajili ya hili ndio [Allah] ametuma Mitume wake, na ameteremsha vitabu vyake, nayo ndio Dini yake ambayo anapenda kutoka kwa waja wake kuidhihirisha, hata lau ndani ya hilo [la kuidhirisha] mtakuwa na kuwauudhi wapinzani wake [Allah amesema:]

(1) Kwa nambari (2516), katika hadithi ya ibnu Abaasi Allah amridhie yeye na babake.

﴿فَٱدۡعُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡكَٰفِرُونَ﴾

{Basi mwombeni Allah mkimsafia Dini Yeye tu, na wangachukia makafiri} [Ghaafir: 14].

Na Allah alimuamrisha Nabii wake swala na salamu za Allah zimshukie awatangazie kaumu yake ya kwamba utume wake umesimama juu ya kumpwekesha Allah kwa Dua,

﴿قُلۡ إِنَّمَآ أَدۡعُواْ رَبِّي وَلَآ أُشۡرِكُ بِهِۦٓ أَحَدٗا﴾

{Sema: Hakika mimi namwomba Mola wangu Mlezi, wala simshirikishi Yeye na yeyote} [Al-Jinni: 20].

# ADHABU YA ATAKAYEFANYA KIBURI CHA KUACHA KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE

Atakayefanya kiburi na kuacha kumuomba Yeye, basi Allah amemuahidi moto na udhalilifu

﴿ وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴾

{kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia jahanamu wadhalilike} [Ghaafir: 60].

Na yule ambaye nafsi yake imechukia kumuomba Allah peke yake, na wala isipate ukunjufu ila kwa kuwaomba viumbe; basi hilo ni alama ya upotevu na kughafilika na Akhera, Allah aliyetakasika amesema:

﴿ وَإِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَحۡدَهُ ٱشۡمَأَزَّتۡ قُلُوبُ ٱلَّذِينَ لَا يُؤۡمِنُونَ بِٱلۡأٓخِرَةِ ﴾

{Na anapotajwa Allah peke yake nyoyo za wasio iamini Akhera huchafuka} [Az-Zumar: 45], yaani: nyoyo zao zilichukia na zikawa na kiburi, na

hazikukubali kumpwekesha Allah peke kwa ibada na maombi.

# DUA NDIO IBADA

Hakuna makamu ya kiimani yeyote aliyoifaradhisha Allah juu ya nyoyo ila Dua imelazimiana nayo.

Na ibada za dhahiri na za batini zote ni Dua katika mwisho wake au maana yake; basi aliyeswali au aliyefunga au aliyefanya hija au aliyetoa sadaka; basi yeye anamuomba Mola wake kwa ulimi wa hali yake, ibada yake kwa Mola wake, udhalilifu wake kwake na mapenzi yake kwake, yanamnadia Mola wake kuwa yeye ni mwenye kuomba kwa Mola wake kukubaliwa, na ni mwenye kutaka ukaribu kwake.

Basi Dua ndio ibada na ndio roho yake, kiini chake na uhakika wake, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

((إِنَّ الدُّعَاءَ هُوَ الْعِبَادَةُ، ثُمَّ قَرَأَ:

﴿ وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡ ﴾)).

«**Hakika dua ndio ibada**», kisha akasoma: {Na Mola wenu akasema: Niombeni nitawaitikia} imepokewa na Ahmad[1].

(1) Kwa nambari (18432), katika hadithi ya An-Nu'maan ibnu Bashiir Allah amridhie yeye na babake.

# UMUHIMU WA KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE

Na kwa ajili ya utukufu wa jambo la Dua na ukubwa wa cheo chake; Allah amefungua kitabu chake kwa Dua:

﴿ ٱهۡدِنَا ٱلصِّرَٰطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ ﴾

{Tuongoze njia iliyonyooka} [Al-Fatihah: 6], na akakihitimisha na kwa 'Al-Muawwidhataini' ambazo mnao ndani yake Dua.

Na Allah akaiita Dua na jina la Dini, akasema:

﴿فَٱدۡعُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡكَٰفِرُونَ ﴾

{Basi muombeni Allah hali ya kumtakasia Yeye Dini} [Ghaafir: 14].

Na akaiita yote na jina la ibada, akasema:

﴿ وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴾

{Na Mola wenu akasema: Niombeni nitawaitikia, kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu

Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike} [Ghaafir: 60].

# KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE NI ALAMA YA IMANI

Kumtakasia Allah peke yake katika Dua ni alama ya imani, na dalili ya yakini, na ni kamba ya uokofu, na njia ya kufuzu na kufaulu, nayo ni alama ya Manabii na waumini.

Basi mwenye kuomba anaye mpwekesha Mola wake katika Dua zake ndiye mfanyi ibada aliye mkweli, na mjuzi aliyesibu njia ya hakika tukufu mno, kwani Dua ndio nguzo imara ambayo waisilamu wanaikimbilia, na ni kinga ya amani ambayo wenye mahitaji hujikinga nayo.

Na misiba na shida humtambulisha mja Mola wake, na humshika mkono kumpeleka kufanya ikhlasi katika maombi yake,

﴿وَإِذَا مَسَّ ٱلْإِنسَٰنَ ٱلضُّرُّ دَعَانَا لِجَنۢبِهِۦٓ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَآئِمًا﴾

{Na mtu akiguswa na shida hutuomba naye kaegesha ubavu, au kakaa, au kasimama} [Yunus: 12].

# ALLAH PEKE YAKE NDIYE MWENYE KUITIKIA MAOMBI

Mola wetu Mlezi aliyetakasika anaombwa peke yake katika kila kipindi na hali; kwani Yeye ndiye Muumba ambaye hashindwi na kitu, na Muweza Mshindi aliyekuwa juu ya kila kitu, riziki ipo mkononi mwake, na kutoa na kunyima kunatoka kwake kunarudi na kwake.

Na Sifa za ukamilifu, uzuri na utukufu ni sifa za kweli ambazo haziepukani Naye, na atakayekutawasali kwake kwa Majina yake na Sifa zake atampa mahitaji yake,

﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَا﴾

{na Allah ana Majina mazuri kabisa, basi muombeni kwayo} [Al-A'raf:180].

Mola wetu Mlezi ndiye aliye karibu na [mja] mwenye kumuomba na kumuabudu, yeyote miongoni mwao anayempelekea haja zake kwake humtekelezea, na atakayemuomba humpatia, na atakaye onyesha ufukara kwake basi humkwasisha

﴿ وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ﴾

{Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba} [Baqara: 186].

Yeye ni Al-Hayyu [aliye na uhai kamili] Al-Qayyuum [anayesimama kwa Nafsi yake na wote wasiokuwa Yeye wanasimama kwa kumtegemea Yeye] anayemuomba amemuelekea Mola Mmoja Mwenye kupelekewa mahitaji yote Muweza wa kufariji majanga,

﴿ هُوَ ٱلْحَيُّ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ فَٱدْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ ﴾

{Yeye ndiye aliyehai - hapana anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye. Basi muabuduni Yeye mkimsafishia Dini Yeye} [Ghaafir: 65].

Na kupwekeka kwa kustahiki kuombwa ni dalili ya kuwa Yeye peke yake ndiye Haki, na kuwa maombi ya kuombwa asiyekuwa Yeye hayaitikiwi, [Allah] iliokuwa kuu shani yake amesema:

﴿لَهُۥ دَعْوَةُ ٱلْحَقِّ وَٱلَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِۦ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُم بِشَيْءٍ﴾

{Wa kuombwa kweli ni Yeye tu. Na hao wanao waomba badala yake hawawajibu chochote} [A-Ra'd: 14].

Vipawa vyake vinapiga akili butwaa, na ukarimu wake ni maajabu makubwa, analipa kwa jema dogo kheri nyingi.

Na atakaye msifu na akaomba kwa vizuri basi [Allah] atamkabili na vipawa vingi, na husamehe madhambi makubwa kwa ambaye Dini yake na Tawhidi zimekuwa sahihi na hakumshirikisha mwengine pamoja naye, [Allah] aliyetakasika amesema katika hadithi kudsi:

((**مَنْ لَقِيَنِي بِقُرَابِ الْأَرْضِ خَطِيئَةً** – أي ذنوبه ملأت الأرض أو قارب ملأها – **لَا يُشْرِكُ بِي شَيْئًا لَقِيتُه بِمِثْلِهَا مَغْفِرَةً**))، رواه مسلم.

«**atakayekutana nami akiwa na makosa yaliojaa ardhi au yaliokaribia kujaa ardhi, na hanishirikishi na chochote basi nitakutana naye msamaha mfano wake**», imepokewa na Muslim[1].

(1) Kwa nambari (2687), katika hadithi ya Abu Dhar Allah amridhie.

# MANABII WANAMUOMBA ALLAH PEKE YAKE

Mja anayependeza zaidi kwa Allah ni aliyemwingi wa kumuomba, na kila imani ya mja, fahamu yake ya Dini na mafungamano yake na Mola wake yatakavozidi; bidii yake ya maombi itazidi katika hali zake zote, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema:

**(لِيَسْأَلْ أَحَدُكُمْ رَبَّهُ حَاجَتَهُ كُلَّهَا؛ حَتَّى يَسْأَلَ شِسْعَ نَعْلِهِ إِذَا انْقَطَعَ؛ شسع نعله: هو أحد سيور النعل)**، رواه الترمذي

«**Mmoja wenu amuombe Mola wake Mlezi maisha yake yote; amuombe hata kamba ya kiatu chake itakapokatika**», imepokewa na Tirmidhi(1).

Sheikhul Islaam amesema: «Na Manabii na watu wema hawajaacha kumuomba Allah maslahi ya Dini yao, dunia yao na akhera yao, basi ni nani huyo asiye na haja ya kumuomba Allah aliyetukuka?! Kisha sifa mahsusi ya mja ni amuombe Mola wake Mlezi, na

(1) Kwa nambari (8-3604), katika hadithi ya Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

sifa mahsusi ya Mola Mlezi ni amuitikie [anayemuomba], basi atakayedhania ya kwamba yeye hahitajii kumuomba Yeye [Allah] hakika atakuwa ametoka katika fungo la uja»[1].

Na shani ya Manabii wa Allah ni wingi wa maombi katika hali zote

﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا۟ يُسَٰرِعُونَ فِى ٱلْخَيْرَٰتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا وَكَانُوا۟ لَنَا خَٰشِعِينَ ﴾

{Hakika wao walikuwa wakiharakisha kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea} [Al-Anbiya: 90].

Moyo wa Zakariyya salamu zimshukie ulitamani mtoto, basi akamwomba Mola wake Mlezi kizazi chema, na akamsifu Mola wake akasema:

﴿ إِنَّكَ سَمِيعُ ٱلدُّعَآءِ ﴾

{Hakika Wewe ni mwenye kusikia sana maombi} [Aalu Imraan: 38], kisha akasimama kuenda katika mihrabu yake, mara tu Malaika wanambashiria Nabii

(1) Ar-Raddu a'la Sh-Shaadhily (uk 57).

kutoka mgongoni mwake, juu ya uzee wa umri wake na udhaifu wa mifupa yake,

Na kaumu ya Nuuh walimkabili Nabii wao kwa kumuasi na kumkadhibisha,

﴿ فَدَعَا رَبَّهُۥٓ أَنِّي مَغۡلُوبٞ فَٱنتَصِرۡ ﴾

{Basi akamwomba Mola wake Mlezi akasema: Kwa hakika mimi nimeghilibiwa, basi ninusuru!} [Al-Qamar: 10], basi Allah akawazamisha wote waliojuu ya ardhi katika mafuriko makubwa isipokuwa waliomfuata [Nuuh] katika waumini,

Na Allah alitutolea kisa cha watu wa pangoni, na kuwa walikuwa vijana wenye Tawhidi, walijua ya kwamba kumwomba Allah peke yake ndio Dini ambayo Allah hakubali Dini nyingine kando na hiyo, basi wakasimama katika kaumu yao wakasema:

﴿ رَبُّنَا رَبُّ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ لَن نَّدۡعُوَاْ مِن دُونِهِۦٓ إِلَٰهٗاۖ
لَّقَدۡ قُلۡنَآ إِذٗا شَطَطًا ﴾

{Mola wetu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi. Hatutamwomba mwabudiwa mwengine kabisa badala yake. Hivyo itakuwa tumesema jambo la kuvuka mpaka} [Al-Kahf: 14],

Na uradi wa waumini ni maombi katika ncha mbili za mchana [asubuhi na jioni] na usiku wa mwisho,

﴿تَتَجَافَىٰ جُنُوبُهُمْ عَنِ ٱلْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ﴾

{Mbavu zao zinaepuka vitanda wakimwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku} [As-Sajdah: 16].

Na kukaa na anayekithirisha kumwomba Mola wake Mlezi na hali yeye ni mwenye kumtakasia Allah amali zake; ni miongoni mwa mambo ambayo Allah alimuamrisha nayo Nabii wake:

﴿وَٱصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ ٱلَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِٱلْغَدَوٰةِ وَٱلْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُۥ﴾

{Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanakusudia Uso wake} [Al-Kahf: 28].

# MANUFAA YA KUMUOMBA ALLAH PEKEE

Manufaa ya Dua ni makubwa, na kheri yake ni yenye kuenea, hunufaika nayo waliohai na waliokufa, na hupata baraka zake mwenye kuomba na mwenye kuombewa.

Nayo [Dua] sababu yenye kuathiri kama sababu nyenginezo, mja huomba kwa kadari ya Allah, na huitikiwa na matakwa ya Allah, basi Dua hukinga na balaa endapo hilo limetangulia katika elimu ya Allah, na huleta kheri, na huokoa kwa idhini ya Allah kutokana na maangamivu.

Kwani amri hutoka kwa Allah na inarudi kwake, hana yeyote kati ya viumbe njia ya kuimiliki.

Na kumwomba Allah kwa ikhlasi ni nuru inayomemetuka, haibakishi mshirika wala mpinzani, wala mshirika wala msaidizi, wala muabudiwa wala Mola ila Allah peke yake, na kwayo [Dua kwa ikhlasi] mwombaji anakuwa mja wa Mola wake, akawa ni mwenye kumpwekesha kwa makusudio, kuadhimisha, mapenzi, hofu, na matarajio, na moyo ukafungamana naye katika yenye kufurahisha na na yaliyo mazito, na ulimi ukaleta Dua katika hali ya ukunjufu na majanga.

# MIONGONI MWA ALAMA ZA MWENYE KUMOWEKESHA MOLA WAKE MLEZI

Na atakayekujua uhakika wa Tawhidi yake basi aangalie ni nani anawomba? Basi atakaye kuwa na ikhlasi katika kumwomba kwake Allah atakuwa amesibu Tawhidi.

Na atakayemwomba asiyekuwa Allah atakuwa ameingia katika shirki, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿ وَمَن يَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرۡهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦٓۚ إِنَّهُۥ لَا يُفۡلِحُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ﴾

{Na anaye muomba - pamoja na Allah - muabudiwa mwenginewe hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hisabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi} [Al-Muminuun: 117].

# MITUME HAWAKUMUAMRISHA YEYOTE KUWAOMBA WAO

Ukamilifu na utukufu ni wa Allah peke yake, na ibada haisilihi kufanyiwa ila Allah, wala kuabudiwa hakustahiki ila kwa utukufu wake.

Na hamna kati ya watu hata wakawa na vyeo vya juu kabisa anayestahiki kuombwa pasina Allah katika machache wala mingi.

Aliyeshindwa kuumba kiumbe kidogo katika huu ulimwengu; basi hana haki ya kuabudiwa na kuombwa,

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ لَن يَخۡلُقُواْ ذُبَابًا وَلَوِ ٱجۡتَمَعُواْ لَهُۥ﴾

{Hakika wale mnao waomba badala ya Allah, hawatoumba hata nzi ijapo kuwa watajumuika kwa hilo} [Al-Haj: 73].

Na Allah ameteuwa kati ya viumbe vyake Mitume na akawafadhilisha juu ya wengine, na wala hamna kati yao aliyeshindana na Allah katika Uola, au aliyeamrisha kuombwa au aliyeridhia hilo,

﴿وَإِذۡ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَى ٱبۡنَ مَرۡيَمَ ءَأَنتَ قُلۡتَ لِلنَّاسِ ٱتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيۡنِ مِن دُونِ ٱللَّهِۖ قَالَ سُبۡحَٰنَكَ مَا يَكُونُ لِيٓ أَنۡ أَقُولَ مَا لَيۡسَ لِي بِحَقٍّ﴾

{Na pale Allah atakapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni waabudiwa kando na Allah? (Na Isa) atasema: Sub-hanaka, Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu} [Al-Ma'idah:116], na walikuwa wanafikwa na maradhi na udhaifu; mna miongoni mwao waliouliwa, na miongoni mwao waliokuwa wagonjwa na waliofanyiwa uchawi, nao ni watu wanakula na kunywa, basi vipi awe muabudiwa ambaye hasimami ila kwa kula chakula?!

Bali kiumbe bora zaidi Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie alivunjwa jino lake la mbele, na akapasuliwa kichwa chake(1), na akaanguka juu ya farasi na ubavu wake ukapuruzika na akaswali kwa kukaa kwa athari ya kuanguka(2).

---

(1) Bukhari, nambari (2911), na Muslim, nambari (1790), katika hadithi ya Sahl ibnu Sa'd Allah amridhie.

(2) Bukhari , nambari (689), na Muslim, nambari (411), katika hadithi ya Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

# KUMUOMBA ASIYEKUWA ALLAH NI DHAMBI KUBWA KABISA KATIKA ARDHI

Kumwomba asiyekuwa Allah ni kosa kubwa, [Allah] aliyetukuka alimwambia Nabii wake swala na salamu za Allah zimshukie:

﴿وَلَا تَدۡعُ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَۖ فَإِن فَعَلۡتَ فَإِنَّكَ إِذٗا مِّنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Na wala usiwaombe wasio kuwa Allah ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa walio dhulumu} [Yunus: 106].

Na katika aina zake kubwa zaidi ni kuchukua wakati baina ya Allah na viumbe wake, sheikhul Islaam amesema: «Hakuna yeyote kati ya Manabii aliyewaekea waja sunnah ya kutaka maombi wala utetezi kutoka kwa watu wema waliokufa, na walioughaibuni, na Malaika, bali hili ndio chanzo cha shirki, kwani hakika washirikina waliwachukua kuwa watetezi, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَيَعۡبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمۡ وَلَا يَنفَعُهُمۡ وَيَقُولُونَ هَٰٓؤُلَآءِ شُفَعَٰٓؤُنَا عِندَ ٱللَّهِ﴾

{Na wanawaabudu wasiokuwa Allah wasio wadhuru wala kuwanufaisha, na wanasema: Hawa ni waombezi wetu kwa Allah!} [Yunus: 18]»[1].

Na dhambi kubwa kabisa katika ardhi ni kumwomba asiyekuwa Allah pamoja naye, ibnu Mas-ud Allah amridhie alisema:

قلت: يا رسول الله أي الذنب أعظم؟ قال: (**أن تجعل لله ندًا وهو خلقك**) متفق عليه

«Nilisema ewe Mtume wa Allah, ni dhambi gani ambalo ni kubwa zaidi? Akasema: **Ni umfanyie Allah mshirika na hali Yeye ndiye aliyekuumba**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[2].

Na Allah amemuonya na adhabu mwenye kumwomba mwengine pamoja na Allah, [Allah] aliyetukuka anasema:

---

(1) Qa'idatun adwiimah (1/121).
(2) Bukhari, nambari (4477), na Muslim, nambari (86).

﴿ فَلَا تَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ فَتَكُونَ مِنَ ٱلۡمُعَذَّبِينَ ﴾

{Basi usimwombe mwingine pamoja na Allah kwa hilo ukawa miongoni mwa watakao adhibiwa} [Ash-Shu'araa: 213], ibnu Abbasi Allah amridhie yeye na babake amesema [akiifasiri aya hii]: Anawaonya wengine [wasiokuwa Mtume] anasema: (Wewe [ewe Muhammad] ni kiumbe mkirimiwa zaidi kwangu, na lau utachukua muabudiwa asiyekuwa Mimi hakika nitakuadhibu)[1].

Na haikuwekwa swala, rukuu, na sijida, wala haikujengwa misikiti katika ardhi ila kwa ajili ya kuombwa Allah peke yake ndani yake, na asiombwe mwengine kabisa, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَأَنَّ ٱلۡمَسَٰجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدۡعُواْ مَعَ ٱللَّهِ أَحَدًا﴾

{Na hakika misikiti ni ya Allah, basi msimuombe yeyote pamoja na Allah} [Al-Jinn: 18].

(1) Tafsiiru Al-Baghawi (3/480).

# MAITI HAMSIKII ANAYEMUOMBA

Mwenye kuomba humuomba Muumba wala hamuombi kiumbe mfano wake, wala haombi uokozi kwa anayeshirikiana naye katika uja, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ عِبَادٌ أَمۡثَالُكُمۡۖ فَٱدۡعُوهُمۡ فَلۡيَسۡتَجِيبُواْ لَكُمۡ إِن كُنتُمۡ صَٰدِقِينَ ﴾

{Hakika hao mnao waomba asiyekuwa Allah ni waja mfano wenu nyinyi. Hebu waombeni, nao wakuitikieni, kama mnasema kweli} [Al-A'raf: 194].

Na aliye kaburini hamsikii anayemuomba hata akimnyanyua hadi katika cheo cha Uola, wala hammilikii anayemtaka uokozi chochote hata akimdaia sifa za muabudiwa,

﴿وَٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمۡلِكُونَ مِن قِطۡمِيرٍ * إِن تَدۡعُوهُمۡ لَا يَسۡمَعُواْ دُعَآءَكُمۡ وَلَوۡ سَمِعُواْ مَا ٱسۡتَجَابُواْ لَكُمۡ﴾

{Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende * Mkiwaomba

hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni} [Faatwir: 13-14],

Na wafu hawana uwezo wa kunusuru nafsi zao, basi ni muhali wawaokoe wengine, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ لَا يَسۡتَطِيعُونَ نَصۡرَكُمۡ وَلَآ أَنفُسَهُمۡ يَنصُرُونَ﴾

{Na hao mnao waomba asiye kuwa Yeye [Allah] hawawezi kukunusuruni, wala hawajinusuru wenyewe} [Al-A'raf: 197],

# MUOMBAJI MAITI ANAYAKINI KUWA [MAITI] HASIKII WALA HANUFAISHI

Mwenye kumwomba asiyekuwa Allah anayakini kuwa anayemwomba hasikii wala hanufaishi, [Allah] aliyetukuka amesema: Ibrahim alisema kuwaambia kaumu yake kuhusu masanamu yao:

﴿ هَلْ يَسْمَعُونَكُمْ إِذْ تَدْعُونَ ۝ أَوْ يَنفَعُونَكُمْ أَوْ يَضُرُّونَ ۝ قَالُوا بَلْ وَجَدْنَا آبَاءَنَا كَذَٰلِكَ يَفْعَلُونَ ﴾

{Je! Yanakusikieni mnapo yaita? * Au yanakufaeni, au yanakudhuruni? * Wakasema: Bali tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo hivyo} [Ash-Shu'ara: 72-74].

Amesema ibnu Kathiir Allah amrehemu: «Yaani: walikiri ya kwamba masanamu yao hawafanyi chochote katika hayo, na hakika si mengine wamewaona baba zao wakifanya hivyo»[1].

(1) Tafsiiru ibni Kathiir (6/146).

# HAMNA KATIKA KUMUOMBA MAITI ILA UCHOFU NA KUHARIBIKA KWA DINI

Atakayemuomba maiti akitarajia kutoka kwake kupata manufaa au kukingwa na madhara; basi hatavuna pamoja na uharibifu wa Dini ila machofu, [Allah] mtukufu wa shani amesema:

﴿ يَدۡعُواْ لَمَن ضَرُّهُۥٓ أَقۡرَبُ مِن نَّفۡعِهِۦۚ لَبِئۡسَ ٱلۡمَوۡلَىٰ وَلَبِئۡسَ ٱلۡعَشِيرُ ﴾

{Humuomba yule ambaye bila ya shaka madhara yake yapo karibu zaidi kuliko nafuu yake. Kwa hakika huyo ni mlinzi muovu, na rafiki muovu} [Al-Haj: 13].

Na mwombaji kuwazungukia viumbe, na kutaka uokozi kwa waliohai na maiti; ni kuidunisha nafsi na kuidhalilisha, imam Ahmad Allah amrehemu amesema: «Ewe Allah, kama ulivouzuia uso wangu na kumsujudia asiyekuwa Wewe; basi ulinde na kumwomba asiyekuwa Wewe, na hawezi kuondoa madhara na kuleta manufaa ila Wewe»[1].

(1) Jaami'ul uluumi wal hikam (1/481).

# ATAKAYEMUOMBA ASIYEKUWA ALLAH KATIKA KUPATA FARAJA YA JANGA LAKE ALLAH ATAMUADHIBU NA JANGA KUBWA ZAIDI

Hakuna mja yeyote atakaye mwomba asiyekuwa Allah au moyo wake ukamgeukia asiyekuwa Allah, au shetani akamtia wasiwasi wa kufumana na asiyekuwa Mola wake Mlezi; ispokuwa atafikwa na shida na majanga yatakayomtambulisha ukosefu wa uwezo wa yule aliyemuua aliyemuomba, na yatakayombainishia udhaifu wake na uduni wake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿قُلْ أَرَءَيْتَكُمْ إِنْ أَتَىٰكُمْ عَذَابُ ٱللَّهِ أَوْ أَتَتْكُمُ ٱلسَّاعَةُ أَغَيْرَ ٱللَّهِ تَدْعُونَ إِن كُنتُمْ صَٰدِقِينَ ۞ بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ إِلَيْهِ إِن شَآءَ وَتَنسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ﴾

{Sema: Mwaonaje ikikujieni adhabu ya Allah, au ikakufikieni hiyo Saa - mtamwomba asiye kuwa Allah, ikiwa nyinyi ni wakweli? * Bali Yeye ndiye mtakaye mwomba, naye atakuondoleeni mnacho

mwombea akipenda. Na mtasahau hao mnao wafanya washirika wake} [Al-An'aam: 40-41].

Na aliyejua kupwekeka kwa Allah katika ufalme, na kutohitajia kwake viumbe; atakata tamaa ya kupata manufaa ila kutoka kwake, na matarajio yake yatakatika ila kumtarajia Yeye

﴿ قُلِ ٱدۡعُواْ ٱلَّذِينَ زَعَمۡتُم مِّن دُونِ ٱللَّهِ لَا يَمۡلِكُونَ مِثۡقَالَ ذَرَّةٖ فِي
ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَلَا فِي ٱلۡأَرۡضِ وَمَا لَهُمۡ فِيهِمَا مِن شِرۡكٖ وَمَا لَهُۥ مِنۡهُم مِّن ظَهِيرٖ ﴾

{Sema: Waite mnao wadaia kuwa ni badala ya Allah. Hawamiliki hata uzito wa chembe katika mbingu wala ardhi. Wala hawana ushirika wowote humo. Wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao} [Saba': 22].

# HALI YA ALIYEMUOMBA ASIYEKUWA ALLAH WAKATI WA KUFA

Pindi mauti yatamfikia aliyekuwa akiabudu wengine pamoja na Allah atakataa aliyoyafanya:

﴿ ٱلَّذِينَ تَتَوَفَّىٰهُمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ ظَالِمِيٓ أَنفُسِهِمۡ فَأَلۡقَوُاْ ٱلسَّلَمَ ﴾

{Ambao Malaika waliwafisha nao wamejidhulumu nafsi zao! Basi watasalimu amri} [An-Nahl: 28], yaani: watadhihirisha kuskiliza, kutii na kuandama wakisema:

﴿ مَا كُنَّا نَعۡمَلُ مِن سُوٓءِۭ ﴾

{waseme: Hatukuwa tukifanya uovu wowote} [An-Nahl: 28].

Na siku ya kiyama macho ya kila mtu yataondokewa na pazia, basi aone ajizi ya viumbe kwa jicho la yakini; na ashuhudie kukataa kwa wale waliokuwa wakiombwa, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَتۡهُمۡ رُسُلُنَا يَتَوَفَّوۡنَهُمۡ قَالُوٓاْ أَيۡنَ مَا كُنتُمۡ تَدۡعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِۖ قَالُواْ ضَلُّواْ عَنَّا﴾

{mpaka watakapo wafikia wajumbe wetu kuwafisha, watawaambia: Wako wapi mlio kuwa mkiwaomba badala ya Allah? Watasema: Wametupotea!} [Al-A'raf: 37], yaani: wametuondokea, basi hatutarajii manufaa yao wala heri zao.

Na atakayemwomba asiyekuwa Allah, Allah ataghadhibikia na amtie motoni milele, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema:

(**من مات وهو يدعو من دون الله ندّاً دخل النار**) متفق عليه.

«**atakayekufa na hali anamwomba asiyekuwa Allah mshirika ataingia motoni**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

---

(1) Bukhari , nambari (4497), na Muslim, nambari (92), katika hadithi ya Abdullah ibnu Mas'ud Allah amridhie.

# MAPENZI YA SHETANI NI KUOMBA ASIYEKUWA ALLAH

Dua ni ibada azizi, kwayo anabainika mtu wa Tawhidi kutokana na asiyekuwa mtu wa Tawhidi, nayo ni katika milango ya rahisi sana kwa shetani kufisidi Dini ya mja, ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: «kutaka mahitaji kutoka kwa wafu, kutaka uokozi kutoka kwao, na kuelekea kwao ndio chanzo cha shirki ya ulimwenguni».

Na Muisilamu huukusanya moyo wake, ibada zake na miamala yake kwa Mola wake peke yake, na hutofautisha katika elimu yake, niya yake, matakwa yake na mapenzi yake baina ya Muumba na kiumbe, akatambua haki ya kila mmoja na cheo chake, wala hampatii mmoja wao anayostahiki mwengine.

Basi Mola Mlezi anastahiki ibada, maombi, hofu na matarajio.

Na waja wema wanastahiki mapenzi, kuandamwa, kuhifadhiwa heshima na kutajwa vizuri. [ALLA] aliyetakasika amesema:

﴿فَأَقِمۡ وَجۡهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفٗاۚ فِطۡرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِي فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيۡهَاۚ لَا تَبۡدِيلَ لِخَلۡقِ ٱللَّهِۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلۡقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعۡلَمُونَ﴾

{Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Allah alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Allah. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui} [Ar-Ruum: 30].

# TAWHIDI NDIO JAMBO AZIZI ZAIDI ANALOLIMILIKI BINADAMU

Jambo ghali zaidi alilopewa mja ni kumpwekesha Mola wake [Tawhidi], na neema adhimu zaidi ni kule kukita kwake juu yake hadi akutane Naye [Allah], kwani uchache wake unaposihi unaokoa na kukaa milele motoni, na ukamilifu wake unazuia kuingia [motoni].

Na anao shetani hila na shubuha anazowatoa kwazo waja wa Allah katika Dini yao, na hakuna shubuha inayomuijia mja ila mnao ndani yake lenye kumghuri aifuate, na linamlingania katika kuisadikisha.

Basi anayetaka salama aichunge Tawhidi yake na imani yake, kwa kusoma Qur-ani na kuizingatia, na ajiandae kwa elimu, na aiepushe nafsi yake na sehemu za shubuha.

Tunamuomba Allah elimu yenye manufaa, amali njema na Dua yenye ikhlasi kwa Allah.

**Na swala na salamu za Allah zimshukie Nabii wetu Muhammad, jamaa zake na masahaba wake wote.**

# FAHARASA YA MAUDHUI

UTANGULIZI ........ 5
UHAKIKA WA DINI YA UISILAMU NI KUMTAKASIA ALLAH AMALI ... 7
DINI YA UISILAMU IMESIMAMA JUU YA KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE ........ 9
ADHABU YA ATAKAYEFANYA KIBURI CHA KUACHA KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE ........ 11
DUA NDIO IBADA ........ 13
UMUHIMU WA KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE........ 15
KUMUOMBA ALLAH PEKE YAKE NI ALAMA YA IMANI........ 17
ALLAH PEKE YAKE NDIYE MWENYE KUITIKIA MAOMBI........ 18
MANABII WANAMUOMBA ALLAH PEKE YAKE ........ 21
MANUFAA YA KUMUOMBA ALLAH PEKEE ........ 25
MIONGONI MWA ALAMA ZA MWENYE KUMPWEKESHA MOLA WAKE MLEZI........ 26
MITUME HAWAKUMUAMRISHA YEYOTE KUWAOMBA WAO ...... 27
KUMUOMBA ASIYEKUWA ALLAH NI DHAMBI KUBWA KABISA KATIKA ARDHI ........ 29
MAITI HAMSIKII ANAYEMUOMBA ........ 32
MUOMBAJI MAITI ANAYAKINI KUWA [MAITI] HASIKII WALA HANUFAISHI........ 34
HAMNA KATIKA KUMUOMBA MAITI ILA UCHOVU NA KUHARIBIKA KWA DINI ........ 35
ATAKAYEMUOMBA ASIYEKUWA ALLAH KATIKA KUPATA FARAJA YA JANGA LAKE ALLAH ATAMUADHIBU NA JANGA KUBWA ZAIDI..... 36
HALI YA ALIYEMUOMBA ASIYEKUWA ALLAH WAKATI WA KUFA.. 38
MAPENZI YA SHETANI NI KUOMBA ASIYEKUWA ALLAH ........ 40
TAWHIDI NDIO JAMBO AZIZI ZAIDI ANALOLIMILIKI BINADAMU... 42

**TAASISI YA TWALIBUL ILM YA KUNUSHURU NA KUGAWA**

**00966506090448**




# Soma katika kitabu hichi:

- Dua ni ibada adhimu sana, muhimu kwa kila Muisilamu, na ikhlasi ndani yake inabainisha kiwango cha Tawhidi ya mja.
- Allah aliyetukuka anapenda kutoka kwa waja wake wamuombe kila wakati, na anambughudhi anayemuombe mwengine.
- Kumuomba Allah peke yake ni miongoni mwa sunnah za Mitume na njia ya mawalii wa Allah wema.
- Kumuomba asiyekuwa Allah miongoni mwa waliohai na wafu ni kumshirikisha Allah, wala muombaji hanufaiki na hili.
- Dhambi kubwa zaidi katika ardhi ni kumuomba asiyekuwa Allah pamoja Naye.
- Tawhidi ndio jambo azizi zaidi analolimiki mja, na atakayeshirikisha katika Dua atakuwa ameikosa Tawhidi.

مترجم بالسواحلية

ردمك:

مؤسسة طالب العلم للنشر والتوزيع: ٠٥٠٦٠٩٠٤٤٨